# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI AMANI MTENDELI**

**S.L.P 03,KAKONKO**

**20/4/2024**

**Mkuu wa Shule -0765856736/0713119387**

**Makamu Mkuu wa Shule-0757841015/0692436207**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI AMANI MTENDELI HALMASHAURI YA KAKONKO MKOA KIGOMA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024.

Shule ya Sekondari AMANI MTENDELI ipo umbali wa Kilometa 20 Kutoka yalipo makao makuu ya wilaya ya kakonko,kwakutokea kibondo shukia kituo

cha mabasi kasanda ambacho kipo kabla ya kufika stendi kuu ya kakonko,lakini kwakutokea nyakanazi kituo cha mabasi kasanda kipo umbali wa kilometa 16 mbele ya stendi kuu ya mabasi kakonko kuelekea kibondo,Usafiri wa pikipiki kutoka kituo cha mabasi kasanda hadi shuleni ni tsh 3000/=(elfu tatu tu)

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 1/7/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 1/7/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/7/2024.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi ya kijani jeshi(sare za darasani),mshono wa LINDABOKSI,(Linda kubwa moja mbele na nyuma na malinda matatu madogo kulia na kushoto) sketi zote ziwe ndefu zinazogusa kiatu.
ii. Mashati meupe mawili mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba)kwa waislamu ni nyeupe ya darasani na zambalau ya kushindia.ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama;
iv. Sare ya Michezo ni tracksout rangi nyeusi yenye mchirizi mweupe.pamoja na raba nyeupe
v. Viatu ya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi pia mwanafunzi aje na mabuti kwaajili ya kujikinga na tope hasa nyakati za mvua;simple na yeboyebo haziruhusiwi,pia aje na kandambili,Taulo na kanga au kitenge kimoja.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe;
vii. Sweta moja rangi ya kijani jeshi lenye nembo ya shule,linapatikana shuleni pia
viii. (Shamba Dress)Skert mbili rangi ya kijivu mshono wa malinda mkeketo nchi moja na nusu kitambaa cha suti.nguo zingne tofauti na zilizotajwa haziruhusiwi kuja nazo,hivyo mwanafunzi aje akiwa amevaa tracksout.
ix. Tai 2 rangi ya sket ya darasani
x. Tisheti (T-shirt) mbili zenye rangi ya kijivu ziwe za kola nyeupe na zenye nembo ya shule,zinapatikana shuleni pia

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 counter Q3 au Q4
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu angalau viwili kila somo kulingana na tahasusi aliyopangiwa;
iv. Godoro Nchi mbili na nusu.pia godoro linakodishwa shuleni kwa bei nafuu kabisa
v. Mashuka Jozi 2 (bluu bahari 1 na pink 1),blanket 1, foronya ya godoro 1, na chandarua 1.
vi. Nguo za ndani za kutosha; pamoja na vifaa vingine kwaajili ya mahitaji yake
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 3(chelewa 1,mopa 1&softbroom 1).
x. Mwanafunzi anapaswa pia kuja na sanduku imara(tranka)kwaajili ya kutunzia vitabu vyake na mali zingine.
xi. Kila mwanafunzi anapaswa kuleta kivuli(kopi na orijino) cha matokeo ya mtihani wa kidato cha nne(resultslip).
xii. Sambamba na mahitaji yaliyooneshwa hapo juu hudumu zote muhimu zinapatika pia katika duka lililopo ndani ya shule.

**NB:Kila mwanafunzi anapaswa kuja na bima ya afya ili kumsadia katika matibabu anapokuwa na changamoto za kiafya.**

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |
| | | |

**Michango yote ya shule ilipwe kupitia akaunti ya Benki;NMB 52110014992 YENYE JINA; AMANI MTENDELI SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT.**

## 3.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**....................................**

**SALOME METHOD KITWE**
**MKUU WA SHULE.**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule -0765856736 AU 0713119387**
- **Makamu Mkuu wa Shule -0757841015 /0692436207**
- **Mwandamizi Taaluma-0763346351**

## HISTORIA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la mwanafunzi(majina matatu)……………………………………………………………..

2. Jina la baba ……………………………………………………………………..

3. Jina la mama………………………………………………………………………

4. Jina kamili la mlezi………………………………………………………………..

5. Anuani ya mzazi/mlezi……………………………………………………………

6. Uhusiano wa mlezi…………………………………………………………...

7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) 8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni……………………………..

9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni........................................................

10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni……………………………………………

11. Afya ya mwanafunzi, Kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

………………………

12. Madhehebu ya dini…………………………………………………………

13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

**Jina kamili Kazi yake Anuani yake (Simu)**

1. ………………………….. …………………………. …………………. 2. ………………………….. …………………………. ………………….....

3. ………………………….. …………………………. …………...........

4. ………………………….. …………………………. …………………

**KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.**

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………

Jina la mzazi/mlezi……………………………………………………………………....

Anuani ya mzazi/mlezi…………………………………………………………………..

Uhusiano…………………………………………...….(mjomba, shangazi, kaka, dada).

Mimi ………………………………………….nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania.

Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni,nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa Nitazingatia na kuhudhuria vipindi siku zote za masomo na nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA UTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi………………………………Tarehe……………….......................

Mimi ………………………………………………………mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………..ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi………………………………Tarehe………………… Page 7 of 11

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Pupil's name…………………………………………………………………………………...

Age ……………………………………………………………………………………………

Stool test……………………………………………………………………………………

Blood group…………………………………………………………………………………...

Urine analysis………………………………………………………………………………….

Sphills test ……………………………………………………………………………….....

Chest test………………………………………………………………………………………

Speech…………………………………………………………………………………………

Eye test ……………………………………………………………………………………….

Abdomen………………………………………………………………………………………

Additional information and physical defect or impairment to pursue further education

…………………………………………………………………………………………………

………

…………………………………………………………...…………………………………………

……

…………………………………………………………

Signed …………………………………………………………………………………

Designation ……………………………………………………………………………

Official stamp

Date ……………………………

**OFISI YA RAISI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA TAMISEMI.**

**SHULE YA SEKONDARI AMANI MTENDELI.**

**AHADI YA MZAZI:**

Mimi……………………………………………………………(Jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………………………………..kidato cha…………………………………….

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema.Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii.Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia mwanangu malezi na elimu bora kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.Na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapo takiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………….

Anuani kamili……………………………………………

Simu……………………………………………………

Tarehe……………………………………………